**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA NYANG'HWALE**

# TANGAZO

TAREHE 30/09/2024

MKURUGENZI MTENDAJI WA HALMASHAURI YA WILAYA YA NYANG'HWALE ANAWATANGAZIA WAKAZI WOTE WA HALMASHAURI KUJITOKEZA KWA WINGI KUSHIRIKI KWENYE MIKUTANO YA JAMII (WANANCHI) KWA KILA KIJIJI KWA VIJIJI VYOTE 62 JUU YA KUREJEA KWA MIKOPO ASILIMIA KUMI KWA VIKUNDI VYA WANAWAKE, VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU.

AGENDA ZA MIKUTANO

1. UTOAJI WA MIKOPO YA ASILIMIA KUMI (10%) KWA VIKUNDI VYA WANAWAKE, VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU ILIYOREJESHWA NA RAIS DKT. SAMIA SULUHU HASSANI.
2. KUJUA MIONGOZO, KANUNI, SHERIA NA TARATIBU MPYA ZA MIKOPO YA YA ASILIMIA KUMI.
3. KUVIJULISHA VIKUNDI VILIVYOKWISHA WASILISHA MAOMBI YA MIKOPO KUWA YAMEFUTWA HIVYO YATATAMBULIWA UPYA KUPITIA MIKUTANO YA SERIKALI ZA VIJIJI.
4. KUVIJULISHA VIKUNDI VYOTE VILIVYOSAJILIWA KWA AJILI YA KUOMBA MKOPO VITATAMBULIWA UPYA KWA KUFUATIA MWONGOZO MPYA WA UTOAJI WA MIKOPO.
5. TAREHE NA TAARIFA YA MKUTANO ITATOLEWA NA VIONGOZI WA VIJIJI HUSIKA.
   VIKUNDI VYENYE MIRADI FURSA HII SI YA KUKOSA ILI KUJIKWAMUA KIUCHUMI NA KUBORESHA UZALISHAJI KUPITIA MIKOPO ISIYOKUWA NA RIBA.

NB. VIKUNDI VINAVYODAIWA MAREJESHO VINATAKIWA KUKAMILISHA MAREJESHO KWA MUJIBU WA MIKATABA, AIDHA WATAKAOCHELEWESHA KUREJESHA NA WANAODAIWA HAWATAKUWA NA SIFA YA KUKOPESHEKA NA WATAWAJIBISHWA KWA MUJIBU WA SHERIA.

- UPATAPO UJUMBE HUU MJULISHE NA MWENZAKO

HUSNA TONI
MKURUGENZI MTENDAJI (W)
NYANG'HWALE

MKURUGENZI MTENDAJI
S.L.P 352
NYANG'HWALE